



# Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Simu: +255 (0)22-2122722/3  
Nukushi: +255 (0)22-2130852  
Barua pepe: [dg@nbs.go.tz](mailto:dg@nbs.go.tz)  
Tovuti: [www.nbs.go.tz](http://www.nbs.go.tz)

18 Barabara ya Kivukoni,  
S.L.P. 796,  
11992 - Dar es Salaam,  
TANZANIA.

Unapojibu tafadhali taja:  
Kumb. Na. NBS/N.20/2/

Tarehe: 9 Oktoba, 2015

## TAARIFA KWA UMMA

### PATO LA TAIFA ROBO YA PILI YA MWAKA (APRILI – JUNI) 2015

#### UTANGULIZI

Ofisi ya Taifa ya Takwimu ina jukumu la kukusanya, kuchakata na kusambaza takwimu rasmi nchini ikiwa ni pamoja na takwimu za Pato la Taifa kwa robo Mwaka. Takwimu za Pato la Taifa hutayarishwa kwa kutumia taarifa za uzalishaji wa bidhaa na huduma zilizo kusanywa kutoka katika vyanzo mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na taarifa za urari wa mauzo nje ya nchi.

Kama mnavyofahamu, Hali ya uchumi iliyotangazwa na Waziri wa Fedha, Mhe. Saada Salumu Mkuya (Mb) wakati wa Bunge la Bajeti la mwaka 2015/16 kuwa thamani ya Pato la Taifa ilikuwa ni TZS. 79.4 trilioni kwa mwaka 2014 ikilinganishwa na TZS. 70.9 trilioni kwa mwaka 2013. Maoteo ya thamani ya Pato la Taifa kwa mwaka 2015 ilikuwa TZS. 89.0 trilioni na Wastani wa Pato la Mwananchi kwa mwaka 2015 linakadiriwa kuwa TZS. 1,828,022.

Katika kipindi cha Januari hadi Juni 2015 Pato la Taifa kwa bei ya miaka inayohusika ni TZS. 45.5 trilioni ikilinganishwa na TZS. 39.0 trilioni za kipindi kama hicho mwaka 2014.

Kutokana na matokeo ya thamani ya Pato la Taifa katika kipindi cha Januari hadi Juni mwaka 2015 ambayo ni 45.5 trilioni ikilinganishwa na maoteo ya Januari hadi Desemba kwa mwaka 2015 ambayo ilikuwa TZS. 89.0 trilioni, inaonyesha kuwa thamani halisi iliyokwishapatikana inazidi nusu ya maoteo. Hivyo tunategemea kuwa kama hakutakuwepo na misukosuko ya kiuchumi inayoweza kuathiri uzalishaji wa mazao na huduma nchini, thamani ya Pato la Taifa halisi itazidi TZS. 89.0 trilioni kwa mwaka 2015.

Lengo kuu la mkutano huu na wanahabari ni kuwaomba muwaelimishe wadau mbalimbali wa takwimu za Pato la Taifa kwa robo ya pili ya mwaka 2015 kuwa:

- ❖ zimetayarishwa na zinapatikana hivyo zitumiwe katika kutayarisha sera na program mbalimbali za nchi; na
- ❖ ndizo takwimu rasmi za Pato la Taifa kwa robo ya pili ya mwaka 2015


### **PATO LA TAIFA ROBO YA PILI 2015**

Takwimu za Pato la Taifa kwa robo mwaka ni thamani ya bidhaa na huduma zilizozalishwa nchini katika vipindi vya miezi mitatu mitatu ambavyo ni Januari – Machi, Aprili – Juni, Julai – Septemba na Oktoba - Desemba.

Thamani ya Pato la Taifa kwa bei za miaka inayohusika katika kipindi cha Aprili hadi Juni ilikuwa TZS 23.6 trilioni ikilinganishwa na TZS 20.4 trilioni kipindi kama hicho mwaka 2014.

Aidha, thamani ya Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2007 katika kipindi cha robo mwaka ya pili ilikuwa TZS. 11.1 trilioni kwa mwaka 2015 ikilinganishwa na TZS 10.3 trilioni katika kipindi kama hicho mwaka 2014, hii inamaanisha kuwa Pato la Taifa liliongezeka kwa kasi ya asilimia 7.9 katika kipindi cha robo ya pili mwaka 2015 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 10.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2014.

**Kielelezo 1: Kasi ya Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Robo ya Pili, Aprili hadi Juni, 2006 – 2015**



## UKUAJI WA PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI

Kutokana na mwongozo wa kimataifa wa utayarishaji wa takwimu za Pato la Taifa, shughuli za kiuchumi, zimegawanywa katika makundi mbalimbali. Ukuaji wa Pato la Taifa kwa robo mwaka ya pili 2015 umeainishwa kulingana na makundi ya shughuli za kiuchumi kama ifuatavyo:

### *Ukuaji wa Sekta ya Kilimo na Mifugo*

Shughuli za kiuchumi za kilimo na mifugo zilikuwa kwa asilimia 4.2 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2015 ikilinganishwa na kasi ya ukuaji wa asilimia 3.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2014.

Ukuaji wa sekta ya kilimo na mifugo ulitokana na upatikanaji wa mvua za kutosha kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo pamoja na ufuatiliaji na udhibiti wa mauzo ya mifugo nje ya utaratibu. Katika kipindi hicho uzalishaji wa mazao ya mahindi uliongezeka kutoka tani milioni 1.59 mwaka 2014 hadi tani milioni 1.64 mwaka 2015. Uzalishaji wa mpunga uliongezeka kutoka tani milioni 0.79 mwaka 2014 hadi tani milioni 0.86 katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Uzalishaji wa maharage uliongezeka kutoka tani 262 elfu mwaka 2014 hadi tani 280 elfu mwaka 2015.

### *Shughuli za Uchumi za Viwanda na Ujenzi*

Pato la Taifa kutokana na shughuli za **Uchimbaji Madini, Mawe** na **Kokoto** ziliongezeka kwa kasi ya asilimia 8.3 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2015 ikilinganishwa na kasi ya ukuaji wa asilimia 6.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2014. Uzalishaji wa dhahabu ulikuwa kg 10,682 ikilinganishwa na kg 9,917 mwaka 2014. Uzalishaji wa Almasi katika kipindi cha robo ya pili 2015 ulikuwa karati 52,928 ikilinganishwa na karati 50,277 mwaka 2014. Madini ya Shaba yaliyozalishwa katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2015 yalikuwa kg 3,854,305 ikilinganishwa na kg 3,686,401 zilizozalishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2014.

Shughuli za **Uzalishaji bidhaa Viwandani** zilikuwa kwa kasi ya asilimia 6.9 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2015 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 10.1 kipindi kama hicho mwaka 2014. Kasi ya ukuaji ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa zisizo za vyakula zikiwa ni pamoja na, nguo, samani, bidhaa za plastiki na bidhaa za kemikali na madawa.

Shughuli ya **Uzalishaji nishati ya umeme** ilikuwa kwa kasi ya asilimia 18.5 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2015 ikilinganishwa na kasi ya asilimia hasi 0.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2014. Kuongezeka kwa ukuaji wa nishati ya umeme kulitokana na kuongezeka kwa umeme uliozalishwa kutoka kwenye mitambo inayotumia, maji. Umeme uliozalishwa katika

kipindi cha robo mwaka ya pili 2015 uliongezeka na kufikia Kwh 1,588.1 kutoka Kwh 1,489.0 uliozalishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2014.

Shughuli za **Ujenzi** ambazo zinajumuisha ujenzi wa nyumba za makazi na zisizo za makazi; barabara na madaraja; na shughuli nyingine za uhandisi katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2015 zilikuwa kwa asilimia 13.2 ikilinganishwa na asilimia 37.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2014.

#### *Ukuaji wa Shughuli za Uchumi za Utoaji Huduma*

Shughuli za **Biashara za jumla na reja reja, Ukarabati wa Magari na Pikipiki na Vifaa vingine vya Nyumbani** zilikuwa kwa kasi ya asilimia 9.5 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2015 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 12.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2014. Shughuli za **Uchukuzi na Uhifadhi** zilikuwa kwa kasi ya asilimia 8.8 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2015 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 9.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2014.

Shughuli ya **Malazi na huduma ya Chakula** ilikuwa kwa kasi ya asilimia 2.1 kwa robo ya pili ya mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 3.0 kipindi kama hicho 2014, shughuli za **Habari na Mawasiliano** zilikuwa kwa asilimia 17.4 katika robo mwaka ya pili 2015 ikilinganishwa na asilimia 18.4 kipindi kama hicho mwaka 2014.

Shughuli za **Fedha na Bima** katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2015 ziliongezeka kwa asilimia 10.4 ikilinganishwa na asilimia 14.2 kipindi kama hicho mwaka 2014. **Upangishaji nyumba** ulikuwa kwa asilimia 2.2 kwa robo ya pili ya mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 2.1 kipindi kama hicho mwaka 2014.

**Huduma za kitaalamu; Kisayansi na Ufundi; Utawala na huduma nyinginezo** zilikuwa kwa asilimia 13.6 robo ya pili ya mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 11.0 ya kipindi kama hicho mwaka 2014.

Aidha, Shughuli za **Utawala wa Umma na Ulinzi** zilikuwa kwa asilimia 8.2 kwa robo ya pili ya mwaka 2015 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.2 kipindi kama hicho mwaka 2014. Huduma za **Elimu** zilikuwa kwa asilimia 6.7 kwa robo ya pili ya mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 5.4 kipindi kama hicho mwaka 2014, huduma za **Afya ya Binadamu** zilikuwa kwa asilimia 8.1 kwa robo mwaka ya pili 2015 ikilinganishwa na asilimia 8.3 kipindi kama hicho

2014 na shughuli za **Sanaa na Burudani** zilikua kwa asilimia 6.6 kwa robo ya pili ya mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 7.0 kipindi kama hicho mwaka 2014, **Huduma nyingine za Binafsi** zilikua kwa asilimia 6.9 kwa robo mwaka ya pili 2015 ikilinganishwa na asilimia 6.7 ya kipindi kama hicho mwaka 2014 na shughuli nyingine za **Kaya zinazoajiri** zilikua kwa kasi ya asilimia 2.6 kwa robo ya pili ya mwaka 2015 ukilinganisha na ukuaji wa asilimia 2.7 kipindi kama hicho mwaka 2014.

Kasi ya ukuaji wa sekta ya Utoaji Huduma imeongezeka kidogo kutokana na kasi ndogo ya uzalishaji wa bidhaa kutoka katika viwanda vya ndani na bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kuuzwa.

## **HISTORIA YA UKUAJI WA PATO LA TAIFA**

Hali ya kukua kwa Pato la Taifa kwa baadhi ya miaka ilikuwa kama ifuatavyo:

- (i) Mwaka 1985 thamani ya Pato la Taifa kwa bei za miaka inayohusika ilikuwa TZS. Bilioni 108.0, idadi ya watu ilikuwa 21,162,000 na wastani wa pato la mwananchi ilikuwa TZS. 5,107;
- (ii) Mwaka 1995 thamani ya Pato la Taifa kwa bei za miaka inayohusika ilikuwa TZS. Bilioni 2,796.6, idadi ya watu ilikuwa 27,472,111 na wastani wa pato la mwananchi ilikuwa TZS. 101,799;
- (iii) Mwaka 2005 thamani ya Pato la Taifa kwa bei za miaka inayohusika ilikuwa TZS. Bilioni 15,965.3 idadi ya watu ilikuwa 36,197,312 na wastani wa pato la mwananchi ilikuwa TZS. 441,063; na
- (iv) Mwaka 2015 thamani ya Pato la Taifa kwa bei za miaka inayohusika inakadiriwa kuwa TZS. Bilioni 89,055.0 idadi ya watu inakadiriwa kuwa 48,716,617 na wastani wa pato la mwananchi linakadiriwa kuwa TZS. 1,828,022.

## **HITIMISHO**

Ofisi ya Taifa ya Takwimu imekamilisha kutayarisha takwimu za Pato la Taifa kwa robo ya pili mwaka 2015 na kuwa takwimu hizi ni rasmi na zitumike katika kupanga na kurekebisha sera mbalimbali za maendeleo nchini. Aidha, takwimu hizi zinapatikana katika Tovuti ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu, [www.nbs.go.tz](http://www.nbs.go.tz)

**Kwa mawasiliano:**

**Mkurugenzi Mkuu,**

**Ofisi ya Taifa ya Takwimu,**

**Dar es Salaam.**